



Ng'ombe wakila majani ya mihogo yaliyokaushwa



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax. 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Watayarishaji:

Kiura J.N., Bimbuzi S. na Mwakina D

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkuu wa Kituo,

KARI-Mtwapa,


S.L.P 16 Mtwapa

Simu: 041-485842/5486207/0202024751

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 50 /2008

Shilingi 20 za Kenya

**Walishe mifugo
majani ya mhogo
wakati wa kiangazi**



Utangulizi

Mhogo ni chakula cha kawaida Pwani mwa Kenya lakini manufaa yake katika lishe ya mifugo hayajatambulika vyema. Majani yake yanaweza kuchunwa nyakati za kukua za mmea na kukaushwa ili kuwapa mifugo malisho wakati wa kiangazi wa Januari hadi Mechi ambapo malisho hufifia. Mihogo inayopendekezwa kwa kuchunia majani ni aina ya Guzo na ya 2836.

Ulimaji

Panda mihogo mwezi wa sita (Juni) ukiacha nafasi ya mita moja kwa mita moja au futi tatu kwa tatu. Chuna majani kwanzia mwezi wa kumi (Oktoba), yaani miezi minne baada ya kupanda halafu uchune kila mwezi au kila miezi miwili.

Kuvuna

Ili kuvuna majani ya kuhifadhi na malisho ya baadaye:

- Tumia kijiti cha futi moja kupima sehemu ya juu zaidi ya kila tawi la mhogo.

- Ng'oa majani yote yaliyo chini ya hiyo futi moja.
- Toa majani yote yaliyomo kwenye matawi wakati wa kuvuna mizizi.
- Tandaza majani kwenye simiti au kwenye kijikaratasi cha nailoni kwa siku tatu ili yakauke kuzuia uharibifu na kupunguza uwepo wa sumu.



Majani ya mhogo

- Hifadhi majani yaliyokauka kwenye gunia/ mifuko au ufunge kama nyasi kavu (*hay*) ukitumai sanduku la kutayarisha nyasi (*hay box*).

Mazao

Kutoka kwa hekta moja majani kiasi kifuatacho chaweza kupatikana.

Nyakati za kuvuna	Kilo za majani	Idadi ya ng'ombe wanaolishwa	Urefu wa kiangazi (miezi)
Kila mwezi	4800	5	3
Kila miezi miwili	3900	4	3
Kila miezi mitatu	3100	3	3

Zingatia: Jinsi majani yaanavyozidi kuchunwa ndivyo kiasi cha mizizi hupungua.

Ulishaji wa majani

Unaweza kutumia vipimo vifutavyo kwa siku kwa ng'ombe wastani mwenye uzito wa kilo 350:

- Kilo 12 za majani mhogo yaliyokaushwa au kilo 4 hadi 6 kama inalishwa pamoja na nyasi kijani au iliyokauka (*hay*).
- Kilo 3 za kapi (*bran*) ya mahindi au vipande vya mhogo.
- Kilo 8 za *Leucaena*, *Gliricidia*, *Clitoria* au *Mucuna* mbichi au 2 zilizokaushwa.
- Gramu 60 za chumvi ya *maclik super*.
- Wapatie mifugo maji safi wakati wote.